# »Kilimo cha vitunguu kuanzia mwanzo hadi mwisho – Sehemu ya 1«

Kilimo cha vitunguu nchini Kenya polepole kinapata umaarufu kutokana na faida yake kubwa. Vitunguu ni mboga zinazolimwa sana nchini Kenya. Vitunguu hivi ni jamaa moja na vitunguu saumu, vitunguu vya chive, vitunguu vya kichina na vitunguu vya shallot. Unanapaswa kuzingatia aina ambayo ni nafuu zaidi.

Vitungu aina nyekundu huuzwa sana na huzalisha sana. Pia huachukua muda mfupi kukomaa, na vikubwa. Kwa hivyo, mkulima anapaswa kuzingatia aina zinazostawi vizuri katika eneo lake.

## Aina za mbegu

Unapojua aina na sifa zake, inakuongoza jinsi ya kupanda vitunguu, kujua nafasi sahihi ya kuacha kati ya mimea.

Unahitaji kujua aina unayopanda, na ni aina gani inayopendekezwa sokoni.

## Kupanda vitunguu

Udongo unapaswa kulimwa ipaswavyo, na hakikisha udongo unaotaka kutumia una rutuba. Vitunguu huhitaji naitrojeni kwa wingi hasa katika hatua ya kutoa majaniaa. Vitunguu pia huhitaji potasiamu nyingi ili kuanza kuweka vitufe. Samadi husaidia kuongeza rutuba ya udongo. Hata hivyo, changanya samadi vizuri kwa sababu mizizi ya vitunguu ni nyepesi sana, mizizi ndiyo inayolisha vitunguu na kuchukua nitrojeni kwenye majani. Mbolea bora zaidi ni samadi ya ng'ombe na mbuzi, ina nitrojeni nyingi.

## Maandalizi ya kitalu

Andaa kitalu vizuri, nitrojeni ni hitaji kuu. Miche ya vitunguu huchukua takriban wiki 6–8 kukua, na kitalu huchukua takriban wiki 6–8 kulingana na eneo. Mwagiliwa maji kwenye kitalu ipaswavyo, panda kwa muachano ufaao ili kuzuia mbegu kujikandamiza. Vitunguu huchukua karibu miezi 3 kwenye shamba.